# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA THELATHINI NA NANE

**28 MEI, 2026**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

### KIKAO CHA THELATHINI NA NANE – TAREHE 28 MEI, 2026

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI MKUU:**

Taarifa ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Iliyokaguliwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

## III. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

### 450. MHESHIMIWA SUBIRA KHAMIS MGALU (BAGAMOYO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini ahadi ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Kasutu itatekelezwa.

### 451. MHESHIMIWA MORRIS JOSEPH MAKOI (MOSHI VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Rau Madukani - Mamboleo - Materuni Km 7.8 kwa kiwango cha lami.

### 452. MHESHIMIWA ISAYA MOSES MNGURUMI (KONGWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza na kusambaza Madawati katika Shule za Jimbo la Kongwa.

## WIZARA YA UJENZI:

### 453. MHESHIMIWA SILVESTRY FRANCIS KOKA (KIBAHA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaendeleza Mradi wa upanuzi wa Barabara ya Dar es Salaam – Morogoro kipande cha Kibaha hadi Chalinze kuwa njia nane.

### 454. MHESHIMIWA JAFARI WAMBURA CHEGE (RORYA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara ya Utegi hadi Shirati kwa kiwango cha lami.

### 455. MHESHIMIWA KANGI ALPHAXARD LUGOLA (MWIBARA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Wananchi walioathiriwa na ujenzi wa Barabara ya Bulamba – Kisorya watalipwa fidia.

### 456. MHESHIMIWA JESCA YUDA MBOGO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya Narco - Dosidosi - Kiteto yenye urefu wa Km 72 kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA NISHATI:**

**457. MHESHIMIWA ARIF SULEIMAN PREMJI (MTWARA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, upi mpango wa kuwekeza kwenye Vituo vya CNG baada ya kuondoa ushuru wa Sh. 382 kwa kilo ili kuhimiza matumizi ya CNG kwenye vyombo vya moto.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **28 MEI, 2026** | **KATIBU WA BUNGE** |

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA